Utume wa Vijana Parokia ya Simanjiro



Fr. Lawrence Muthee, SVD

1080P
REC
60 MIN
00:00:00:00

“JINSI YA KUTAWALA NAFSI KWA MAFANIKIO YA KESHO”

Semina Maalum

17.06.2023

Kuwa makini na fikira zako

“Uwe makini **unachokifikiria**, kwa sababu

Fikira zako zitageuka kuwa **maneno** unayoyasema,

Maneno yako yatageuka kuwa **matendo**,

Matendo yako yatakuwa **desturi** yako,

Desturi yako itakuwa **tabia** yako

na tabia yako itakuwa **hatima** yako”

TAFAKARI

- "KAMA UNAUMIA NDANI KWA SABABU YA KITU AU JAMBO AMBALO WATU WENGINE WAMESEMA AU KUTENDA, MAUMIVU HAYO SIO KWA SABABU YA KITU AU JAMBO LENYEWE, BALI NI KWA SABABU YA TAFSIRI AU MWITIKIO WAKO KULIHUSU. UNAWEZA KUTENGUA MAUMIVU HAYO MUDA WOWOTE UKITAKA"

Mjadala

Adhari za Mazingira

1. Je, Mazingira tunayoishi na kukuwa yana adhiri tabia zetu? (Ndiyo au la). Kama ndiyo, kwa njia zipi? Kama Hapana, kwa nini?
2. Je, watu tunaoishi nao, wanafamilia, marafiki, wenzetu kazini, makundi ya mtaani, kanisani, nk, yanaadhiri fikira zetu kuhusu Maisha? Kama ndiyo vipi? Kama Hapana, kwa nini?
3. Je, Mambo tunayosoma kwenye mitandao yanaadhiri fikira zetu au la?
4. Je, Mithali isemayo, ukitembea na mwizi siku moja utaiba pia, ni kweli au uongo?
5. Je, Mithali isemayo, sikio la kufa halisikii dawa ina maana gani?
6. Je, Mithali isemayo, ukiona vyaelea ujue vimeundwa ina maana gani?

Wednesday, September 7

Semina ya
Neno la Mungu
Imeandaliwa Na
Mbeya Moravian Town Choir
{kampuni}
01 June to 04 June
Kanisa La Moravian
Mby Mjini Sokomatola
Art By Jeipro
PASTOR
DANIEL MGOGO
ATA HUDUMU
PASTOR
EDWIN MWAKALINGA
MWENYEJI
MBEYA MORAVIAN TOWN CHOIR
WATAIMBA
FILMIGO

Jinsi ya Kutawala nafsi kwa manufaa ya kesho
Ujuzi wa kutatua shida
Ujuzi wa kutangamana
Uzalishaji au uchangiaji
Ubunifu
kujituma
Kujiongeza
uadilifu
kujiamini
Dhabiti
Uwezo wa kuchambua
Kujiendeleza, elimu, ujuzi
Uwezo wa mawasiliano
Nidhamu
Uvumilivu
Uaminifu
Mabadiliko
Subira

UJUZI WA KUTANGAMANA

- KUTANGAMANA NA WATU (INTERPERSONAL SKILLS) – KUTANGAMANA NA WAZAZI, NDUGU, MAJIRANI, MARAFIKI WA KIKE AU KIUME, WAKUBWA, WADOGO, WALIMU, SERIKALI, MWAJILI, VIONGOZI WA DINI, NK.
- KUTANGAMANA NA MAZINGIRA – KAZINI, HALI YA HEWA, MWANGA, GIZA, NK.

UJUZI WA KUTATUA SHIDA

- NI MBINGUNI TU TUNAPOAMINI KWAMBA HAMNA SHIDA NA MATATIZO. MRADI TUPO DUNIANI TUTAKUMBWA NA MATATIZO MAKUBWA NA MADOGO
- NI MUHIMU SANA KUJIFUNZA NJIA TOFAUTI TOFAUTI ZA KUTATUA MATATIZO.
- KATIKA KAZI ZA USIMAMIZI TUNAKUMBANA NA CHANGAMOTO MBALIMBALI.
- KINACHOMFANYA MTU AFAULU KATIKA MAJUKUMU NI UWEZO WA KUTATUA MATATIZO YA KILA SIKU KWA KUJENGA BADALA YA KUBOMOA.
- KUNA NJIA NYINGI ZA KUMUUA PAKA ANAYESUMBUA NA KUHARIBU VITU NDANI: UNAWEZA KUMTAFUTA PEKE YAKO, AU KUOMBA MSAADA WA MARAFIKI, KUMWEKEA MTEGO AU DAWA, AU PIA UNAWEZA UKAICHOMA NYUMBA YULE PANYA AKAFIA NDANI. AMUA NI IPI NZURI.

Uzalishaji au uchangiaji

- Ili jamii iweze kusonga mbele kimaendeleo, kila mwanadamu, awe mtoto, mtu mzima au mzee, anapaswa kuchangia kiasi sawa au Zaidi ya kile anachokula au kutumia.

- Familia na jamii inapokuwa na watu wengi ambao hawafanyi kazi yoyote kuzalisha au kuchangia ufilisika haraka na kubaki maskini.
- Kuzalisha sio lazima ulete hela taslimu. Unaposhirikiana kufanya kazi unapunguza mzigo kwa wengine. Ikiwa Watoto watawajibika kupalilia shamba, wazazi wataokoa gharama za kupalilia na kufanya mambo mengine kama kuboresha makazi.

Ubunifu

Ubunifu utokana na tafakari ya kina. Mungu amempa mwanadamu uwezo kama wa kwake alipompulizia uhai wake (Mwa 2:7).

Watu wengi hasa vijana hawapendi kutafakari. Wanaogopa kutafakari hivyo wanajaza muda ambao hawana kazi maalum kwa burudani hasa kupitia simu janza (TikTok, WhatsApp, Facebook, Instagram, YouTube, etc). Burudani hii sio bure kwa sababu wanahitaji vifurushi vya data ili kuingia mtandaoni. Ukihesabu gharama wanazotumia "kustreem" utashangaa.

Hata hivyo vijana wengine wanatumia mitandao hiyo hiyo kubuni "content" ambayo ukiangalia sehemu ya malipo ya data yako yanaenda kwao.

Kujituma

- vijana wengi ukosa ajira kwa sababu hawapendi kujituma. Hata wakipewa kazi ni mpaka kusukumwa au kusimamiwa.

Wengi wanapenda kukaa tu lakini wapate hela ya kujiunga na data ya mitandao.

Wengi wanapoteza muda mwingi wa Maisha yao “kula bata”

Watu wanaojituma hawakosi kazi.

KUJIONGEZA

- DUNIA YA LEO USIPOJIONGEZA UTAACHWA KWENYE MATAA
- SIO LAZIMA UAMBIWE KILA KITU, UNAHITAJI KUSOMA ALAMA ZA NYAKATI NA KUJIONGEZA. MF. KAMA RAFIKI YAKO AMEACHA KUKUJULIA, HAPOKEI SIMU, HATAKI STORI NYINGI NA WEWE, SIO LAZIMA AKUAMBIE KWAMBA UJIPANGE.
- UKIKUMBANA NA CHANGAMOTO YOYOTE, KWANZA JARIBU KUITATUA MWENYEWE UKISHINDWA OMBA MSAADA.

Uadilifu

Ni sifa ya uaminifu. Mtu mwadilifu ni yule hashukiwi au kusingiziwa maovu. Mtu ambaye anajulikana kwamba hawezi kutenda kinyume. Unaweza kumtuma apelike hela na ukaamini kwamba zitafika

Vijana wengi sio waadilifu hivyo hamna mtu anayeweza kuwaaminisha kitu. Mf. Ukimpa simu yako angaalie picha moja anaanza kuslide kuangalia zingine – udaku

Mtu mwadilifu anapewa majukumu makubwa.

KUJIAMINI

- UWEZO WA KUSIMAMA IMARA KATIKA JAMBO BILA KUTAPATAPA
- KUNA KUJIAMIN CHANYA NA HASI
  - **CHANYA** NI KULE KUWEZA KUSIMAMIA UKWELI BILA KUBABAISHWA NA MANENO YA WATU. NI UWEZO WA KUPOKEA MAJUKUMU NA KUYATEKELEZA BILA UOGA
  - **HASI** NI KULE KUWA NA KIBURI NA KUNG'ANG'ANIA KITU HATA KAMA INAONEKANA WAZI KWAMBA HAUPO SAHIHI AU HAUWEZI – HII INASABABISHA AJALI, AIBU AU UGOMVI. MF. KUNG'ANG'ANIA KWAMBA NAWEZA KUENDESHA GARI.

UDHABITI

- Uimara katika jambo au katika Maisha
- Kupambana na hali zote ili kufikia malengo chanya bila kuteteleka.
- Mtu mwenye udhabiti anasimamia mambo yake vizuri. Sio rahisi kupata mpenyo kwenye maneno au matendo yake.

UWEZO WA KUCHAMBUA

Ukipewa kikapu kilichojaa machungwa mazuri na machungwa mwitu uchambue, lazima uwe unajua mwonekano wa machungwa mazuri na wa machungwa mwitu, la hujui, hautaweza kuyachambua, utachanganyikiwa

Vijana wengi hawajui kuchambua ni mambo yepi yalio na tija katika Maisha yao na ni yepi yalio na madhara.

Mf. Vijana wengi ushawishika kuingia kwenye makundi mabaya, ulaibu wa pombe na mihadarati kwa sababu hawajajengewa uwezo wa kuchambua mema na mabaya.

Akili yao inawapelekea kuchagua mambo ambayo ugeuka karaha.

Kujiendeleza

Vijana wengi hawapendi kujiendeleza kimaisha kwa fani zao au karama na vipaji vyao. Wao ubweteka tu baada ya kupata yale ya msingi.

Wengine wakifeli mtihani wa darasa la saba au kidato cha nne huwa ndo mwisho wa masomo kwao.

Wengine wakihitimu chou basi, hawagusi kitabu wala kutaka kuongeza hekima.

Dunia ya leo inakwenda mwendo kasi sana. Bila kujiendeleza vijana wengi wataachwa nyuma katika dhiki

Mawasiliano

Tunaelewa au kutoelewa jambo kulingana na jinsi mawasiliano yalivyofanyika

Au hatuwasilishi ujumbe vizuri au hatuelewi lugha, ishara au njia ya mawasiliano husika.

Ukitaka watu wakuelewe, lazima ujifunze kuwasilisha ujumbe wako

Kama mawasiliano yako ni mabaya watu watakutafsiri tofauti na ulivyokusudia. Ukisema ndiyo ileweke ni ndiyo na ukisema la ieleweke ni la.

Pia usiridhike na tafsiri moja tu ya jambo. Jaribu upande wa pili. Mara nyingi tunakwasika kwa kuwatafsiri wengine vibaya kulingana na hali, mtazamo au uhusiano tulionao.

NIDHAMU

- Nidhamu ni uwezo wa kujisukuma kufanya kitu kizuri hata kama ni kigumu ili kufikia malengo mf. Kujinyima usingizi ili kusoma au Kwenda kazini.
- Kujinyima burudani ili kuwekeza katika mradi wa manufaa kwako
- Kuachana na makundi ambayo hayana tija kwako
- Kujizuia kusema watu au maneno kuhusu watu
- Kujizuia kula au kunywa kupita kiasi
- Kuzuia hasira au kuropokwa maneno ovyoovyo

UVUMILIVU

Uvumilivu ni wezo wa kupambana na hali ngumu inayobidi mf. Kuvumilia changamoto kv. masimango katika sehemu ya kazi, kwenye ndoa au mahusiano, kazi ngumu ukijua kwamba mwisho utashinda.

Watu wengi wamepoteza ajira, wenzi wa ndoa, kushindwa kuwekeza kwa kukosa uvumilivu.

Lakini kuna hali zingine sio za kuvumilia kv. Uonevu, vita hatarishi ndani ya mahusiano, nk.

Uaminifu

Kuna msemo unaosema uaminifu ni mtaji. Uaminifu ni mojawa wapo wa vitu vya dhamani Zaidi maishani. Mtu mwaminifu anapata fursa nyingi za kujiendeleza katika Maisha

Kusema mimi ni mwaminifu haitoshi, pia uaminifu wa siku moja moja haukubaliki. Au mtu ni mwaminifu au si mwaminifu.

Uaminifu unategemea sana makuzi ya mtu na nidhamu ya kutosheka na kilicho chake halali.

Uaminifu ni kitu ambacho kikivunjika hakiwezi kikakarabatiwa kikarudi kama mwanzo, lazima kovu litaachwa. Huchukua muda mrefu sana na jitihada nyingi kurudisha asilimia Fulani ya uaminifu unapovunjika. Ushauri ni kwamba usiharibu Zaidi, rekebisha.

Tadhmini ya uaminifu katika mahusiano

Kwa wale ambao wapo katika mahusiano	Je, unamfahamu mwenzako vizuri, Zaidi ya jina, anakotoka, unajua umri wake, familia yake, hali yake ya kiafya?
	Je, Unajua amekuwa na mahusiano mangapi ya awali kabla hamjakutana?
	Je, unajua nia yake kuwa na wewe, ni upendo, masilahi, tamaa au malengo ya muda mfupi au mrefu?
	Je unajua kama ni wewe tu upo katika Maisha yake au kuna wengine? Kama ndiyo unaridhia?
	Je, unajua mpango wa Maisha wa mwenzako au uenda “anakula bata” tu kwako?
	Je, ni adhari zipi zinakukondolea macho ikiwa haumfahamu vizuri?

SUBIRA

- Subira uvuta heri. Subira ni siraha kubwa sana. Ukitaka mambo yatulie yenyewe bila kutumia nguvu nyingi kuwa na Subira
- Subira urekebisha mambo mengi na kutatua migogoro mingi.
- Wape watu nafasi wajipike, wajipakue na wajile, watakuacha na amani yako.
- Usiwe mwepesi kutaka kuonyesha watu wewe ni nani. Haisaidii kitu bali uleta ugomvi usiokuwa na maana na wakupoteza muda
- Subira upunguza au kumaliza maumivu. Ukipata hasira usifanye maamuzi muda ule ule, subiri kesho ifike, utakuwa na mawazo tofauti kabisa. Wengi wamejutia kukurupuka kwa hasira.

Adhari za mahusiano bila mpango

1. Hamna sababu ya kudumu – mara nyingi ni anasa tu
2. Hamna dhamana ya Maisha ya mtu mwingine isipokuwa masilahi ya muda mfupi
3. Hamna mpango maalumu kuhusu vipengee vya Maisha kama, afya, lishe bora, masomo, uwekezaji, Imani, uwajibikaji
4. Uzazi bila mpango
5. Kero za mara kwa mara
6. Vita vinavyosababisha majeraha ya kisikolojia, hisia, mwili na hata kifo
7. Kupoteza muda muhimu wa kujiwekeza katika taaluma au maendeleo.



MABADILIKO

- - KUNA MSEMO USEMA "ASIYEBADILIKA NI MJINGA". MABADILIKO NI CHANJA NI KITU KIZURI NA CHA LAZIMA KATIKA MAISHA YA MWANADAMU
  - MSEMO MWINGINE "UKITAKA KUBADILISHA DUNIA, BADILIKA MWENYEWE"
  - HUWEZI KUWABADILISHA WATU WENGINE ILA NI RAHISI SANA KUBADILISHA NAFSI AU MAZINGIRA YAKO.
  - USIOGOPE KUBADILISHA HALI AU TABIA MBAYA KWA KUWAOGOPA WATU. MAISHA NI YAKO.
  - UKITAKA KUPATA AMANI, SIGOMBANE AU KUSHINDANA NA WATU, BADILISHA NJIA AU MAHALI.
  - USIOGOPE KUPOTEZA MASHABIKI KWA KUBADILIKA.

Maswali ya tadhmini

1. Nimejifunza kitu chochote cha maana leo au nimepoteza muda wangu bure kuja hapa? Kama ndiyo, nini? Kama hamna kwa nini?
2. Je, kuna mambo ambayo nimeona nahitaji kubadilisha au kuongeza nguvu katika Maisha yangu? Kama ndiyo, yepi?
3. Je, kuna mambo ambayo naona nahitaji msaada wa ushauri ili kuyaweka sawa katika Maisha yangu? Kama ndiyo, yepi?
4. Je, kwa kuweka alama, 1-10, semina ya leo imeniongezea ufahamu kiasi gani?
5. Je, naweza kuhudhuria semina kama hii tena au kumshauri mtu kuhudhuria? Kwa kiasi gani 1-10?

Asante

Fr. Lawrence Muthee, SVD